**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA KONGAMANO LA KITAIFA LA MAENDELEO YA SEKTA YA HABARI TANZANIA NA KIKAO KAZI CHA MAAFISA HABARI WA SERIKALI TAREHE 18 JUNI, 2024**

- *Mheshimiwa NAPE MOSES NNAUYE (Mb), Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;*

- *Mheshimiwa TABIA MWITA (Mb), Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;*

- *Mheshimiwa MOHAMED MCHENGERWA (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa);*

- *Mheshimiwa JENISTA MHAGAMA (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu);*

- *Mheshimiwa Balozi Dkt. PINDI CHANA (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria;*

- *Mheshimiwa Dkt. DAMAS NDUMBARO (Mb), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo;*

- *Mheshimiwa Mhandisi MARYPRISCA WINFRED MAHUNDI (Mb), Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Tekinolojia ya Habari;*

- *Ndugu MOHAMMED KHAMIS ABDULLA, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; pamoja na Makatibu Wakuu mbalimbali mliopo hapa;*

- *Waandishi wa Habari, Watoa Mada na Washiriki wa Kongamano;*
- *Viongozi wa Dini;*
- *Wageni Waalikwa;*
- *Mabibi na Mabwana;*

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania....................!**

Nami niongeze sauti yangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai, uzima, neema ya sisi kukutana hapa leo kwa jambo hili tunalolifanya.

Nikushukuru Mheshimiwa Waziri Nape kwa kunialika kushiriki Kongamano hili muhimu sana kwa tasnia ya habari nchini. Lakini vilevile, niipongeze Wizara na wote waliohusika na maandalizi mazuri ya Kongamano hili. **Hongereni sana.**

Kabla sijaendelea, naomba niwape rambirambi zangu wanahabari wote kwa kuondokewa na mwenzenu, **Balozi Ferdinand Ruhinda,** aliyefariki tarehe 14 Juni, 2024. Marehemu Ruhinda alihudumu kwenye vyombo mbalimbali vya Serikali, na alikuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa tasnia hii nchini. Sasa pamoja naye, kuna kifo kimetokea na kimenigusa sana. Ni kifo cha mtoto mdogo mwenye ualbino, alikuwa anacheza nyumbani, akatekwa, wamekwenda wamemnyofoa viungo,akuonekana kwa muda wa siku tatu, ameonekana

ameshaharibika. Sasa, naomba tusimame dakika moja tuwaombee. **Mwenyezi Mungu azilaze roho yao mahali pema peponi, Amina**

*Ndugu zangu,* niwashukuru pia wadau wa sekta hii kwa mwitikio mkubwa wa kuhudhuria tukio hili. Nilipoingia nilidhani nitakuta nusu ya waliokuwepo, lakini nilipoingia nikakuta, ukumbi umejaa. Kwa hiyo *nawashukuru pia*, na hii inaonesha kwamba Sekta hii ina mshikamano na mnafanya kazi kwa pamoja. Nimefurahishwa na ushiriki mpana wa wadau mbalimbali wa sekta binafsi pia, asasi na jumuiya mbalimbali za wanahabari. Hii ni ishara kwamba, Wizara inafanya kazi kwa karibu na wadau wake.

Nitumie fursa hii pia kuwapongeza wanahabari waliochaguliwa au kupata Tuzo mbalimbali kimataifa. Naomba niwatambue wachache, ambao baadhi yao nimewaona wako hapa;

(i) **Bi. Beatrice Bandawe** aliyepata Tuzo ya Mwanamke Kiongozi katika Chombo cha Habari kutoka Umoja wa Magazeti Duniani (WAN-IFRA). Ni mara ya kwanza Tuzo kama hii kutolewa kwa Mtanzania. **Tunamshukuru sana.**

(ii) **Bw. Ernest Sungura**, aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kwanza wa Mtandao wa Mabaraza Huru Afrika (NIMCA); Asante sana kwa kutuheshimisha.

(iii) **Bw. Deodatus Balile**, aliyechaguliwa kuwa Rais, wa Jumuiya ya Wahariri Mashariki mwa Afrika (EAES); na

(iv) **Bw. Kajubi Mukajanga**, ambaye alichaguliwa kuongoza Baraza la Vyombo vya Habari Afrika Mashariki (EAPC).

Sasa, hawa kwa niaba ya wote wengine tunawashukuru sana kuiwakilisha Tanzania vizuri. Mafanikio hayo yanatokana na uwezo wenu, vilevile ni utambuzi wa mchango wenu katika tasnia hii kwa ujumla. Hongereni sana kwa kuaminiwa na kupewa Tuzo na nafasi hizo. Endeleeni kuwa Mabalozi wetu.

Pia, nishukuru mashirika yote, NMB, Vodacom na wengine wote waliofadhili shughuli hii, lakini wanaoendelea kuwashika mkono waandishi wa wanahabari katika kazi zao mbalimbali.

Niungane na Waziri nami kumshukuru Bw. Mobhare Matinyi, kwa kazi nzuri aliyoifanya akiwa Msemaji Mkuu wa Serikali. Niwaahidi tu kwamba, ataendelea kuwa nanyi, nitamtumia kwingine lakini muda baada ya muda atakuwa nanyi kuongeza msukumo.

***Ndugu zangu Wanahabari,***

Mimi binafsi siamini katika ukiritimba wa mawazo au fikra (***monopoly of ideas***), ninaamini katika kusikiliza sauti na mawazo ya wenzangu. Mtakumbuka kuwa, siku chache tangu kukabidhiwa dhamana ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nilikutana na kubadilishana mawazo na wahariri wa vyombo vya habari. Nawakumbuka waliokuwepo, alikuwepo Balile, Machumu, Kibanda, na wengine. Katika mkutano ule waliuliza maswali mengi sana lakini ukiwasoma maswali yao walikuwa kama, *"Hivi utafanya nini? Hivi utaweza kweli? Hivi itakuwaje?"* Sasa nadhani majibu sasa wanayo. Lakini nilikutana nao na kubadilishana nao mawazo, ambapo niliwahakikishia ushirikiano mkubwa na

kuwaahidi kulinda uhuru wa waandishi wa habari lakini pia uhuru wa vyombo vya habari kwa ujumla.

Leo hii najisikia fahari kwamba, uhusiano baina ya Serikali na vyombo vya habari unaendelea kuimarika. Yale malalamiko ya hapa na pale kwa kiasi kikubwa yamepungua. Nimesoma Taarifa ya Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA) ya mwaka 2023, kwenye Taarifa iliyowasilishwa na MISA Tawi la Tanzania (MISA-Tan), wamekiri kwamba uhuru wa vyombo vya habari nchini umeimarika sana katika kipindi hiki.

Ninayakumbuka sana maneno ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa India, Mheshimiwa Jawaharlal Nehru, ambaye alisema, nami nakubaliana naye, alisema, "***Nikiambiwa kuchagua kati ya uhuru wa vyombo vya habari, pamoja na changamoto zake katika kuutumia uhuru huo, bado nina hiyari ya kuuchagua uhuru wa vyombo vya habari, kuliko kufinya uhuru wa vyombo hivyo".*** Hayo ni maneno ya Waziri Mkuu Nehru, ambayo na mimi nakubaliana nayo kwa asilimia mia. Hii ni kwa sababu, vyombo vya habari vikiwa huru, vinagusa kila pembe ya maisha yetu. Vinafanya kazi muhimu ya kutoa taarifa zinazoelimisha, kuamsha na kuandaa umma kwenye mambo fulani, vinahamasisha kupokea ujuzi mpya, taarifa za maendeleo ya kiteknolojia katika sekta za uzalishaji lakini pia maendeleo na ustawi wa ya jamii zetu. Vinafichua maovu na kutowajibika kunakofanywa na watumishi na watendaji wa Serikali. Vinatoa mrejesho wa hisia na mawazo ya wananchi kwa Serikali yao, lakini pia, vinafanya kazi ya

kuelimisha na kukuza demokrasia. Hivyo ni vyombo vya habari, vikipewa uhuru wa kufanya kazi yao.

Haya ndio mambo yanayoifanya Serikali kujenga na kuimarisha uhusiano mwema na vyombo vya habari. Vyombo vya habari ***si mshindani wa Serikali, bali ni mdau na mshiriki muhimu wa shughuli za Serikali***. *Huko nyuma kuna kipindi fulani, vyombo vya habari na Serikali vilikuwa vinavutuna, wao wanavuta, nanyi mnavuta lakini tuliona hatukufika pahali si ndiyo katika kipindi hicho. Kwa hiyo hatukufika pahali pazuri sana. Lakini tulipoamua kukaa kitako, kuzungumza, tukaamua kufanya kazi pamoja vyombo vya habari na serikali angalau tunaona na taarifa mbalimbali za kiulimwengu zinasema mengi kuhusu maeneo hayo.* Sasa niseme, kwa maana hiyo, Serikali haina budi kuweka mifumo ya Kisera, Kisheria na Kitaasisi, katika kuimarisha uhuru na mazingira ya kazi ya vyombo vya habari; na hiyo ndiyo kazi ambayo Serikali tunaifanya.

Ninyi ni mashahidi kwa jinsi Serikali inavyoshughulikia kero za muda mrefu zilizokuwa zikiikabili sekta hii muhimu nchini. Machache yaliyobaki yataendelea kufanyiwa kazi kwenye mapitio ya Sera ya Utangazaji na marekebisho ya sheria zinazohusu sekta hii. Nimeyasikiliza mengi yaliyosemwa hapa na timu iliyotafiti hali ya uandishi wa habari, basi yote tutakwenda kuyaangalia na nitalizungumza baadaye.

Lakini kama wanavyosema Waingereza kwamba, ***it takes two to tango,*** wito wangu kwa vyombo vya habari ni kuendelea kutumia uhuru wao kwa weledi na kwa kuzingatia ile dhana ya uandishi wa habari wenye uwajibikaji

(***responsible journalism)*** ndiyo wito wangu kwenu**.** Serikali itafanya yetu, lakini nanyi chezeni wenu.

Pamoja na wito huo, nivishukuru sana vyombo vya habari hapa nchini kwa jinsi vinavyoshirikiana na Serikali katika kutoa habari kwa umma kuhusu masuala mbalimbali yanayoendelea kwenye jamii yetu, ikiwemo harakati za maendeleo na hata majanga yanapotokea, kama mlivyofanya wakati wa maafa ya Hanang na wakati wa mvua za *El-nino* ambazo zimekwisha hivi karibuni, zilizoleta mafuriko kule Rufiji na maeneo mengine nchini. Kupitia kalamu na sauti zenu, umma ulitambua na kuelewa hatari iliyokuwa mbele yetu na kuchukua tahadhari stahiki. Kupitia sauti zenu, juhudi za uokozi zilifanyika kwa uharaka sana na kwa weledi, lakini vilevile tulipata michango mingi kutoka kwenye sekta ya wafanyabiashara na kwengineko, lakini yote ilisababishwa na sauti zenu. Kalamu na sauti zenu, kuandika kina na kima cha athari tuliyoipata wakati ule.

***Ndugu zangu washiriki wa Kongamano hili;***

Ni dhahiri kwamba, vyombo vya habari vinapitia mapinduzi ya utendaji kazi, kutoka tulivyozoea kufanya kazi zetu na kuelekea kwenye matumizi ya teknolojia mpya zinazoibuka kila uchao. Hapa inakuja changamoto ya vyombo vya habari kutoweza kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia lakini pia kitaaluma, kiujuzi na kiuchumi pia, kama ilivyosemwa hapa. Kila leo mabadiliko ya teknolojia yanakuja, lakini kasi ya vyombo vyetu kuendana na mabadiliko

yale ni ndogo, na ni ndogo kwa sababu labda tuna mapungufu kwenye utaalamu, ujuzi lakini pia kifedha, kiuchumi, hatuko vizuri sana.

Aidha, vyombo vya habari ulimwenguni vinarasimisha maudhui ambayo katika maeneo mengine ya dunia yanakuwa ni tishio kwa mila, desturi na heshima za jamii za maeneo hayo lakini pia hali za kisiasa za maeneo hayo. Vyombo vyetu nchini vina wajibu wa kulinda hayo na sio kuhamasisha kwa kisingizio cha biashara. Amegusia kidogo Bw. Tido Mhando, aliposema kwamba, kuna wakati vyombo vya habari vinashughulika na masuala madogo (*trivial issues)* kufanya matangazo madogo madogo, havingii kwenye ufafanuzi/uchambuzi wa masuala wanayoyatangaza hususan masuala ya kisiasa, kwa sababu ya kuogopa kushughulikiwa. Wakati mwingine vyombo vya habari vinajishughulisha kwenye mambo hayo, kwa sababu za kibiashara tu, kuingiza pesa. Kwa hiyo, hizo ndiyo changamoto ambazo mimi ninaziona. Kwamba, uwezo, taaluma na ujuzi wa vyombo vyetu ndivyo vinavyochangia tujielekeze kwenye masuala madogo madogo yasiyo na tija.

***Ndugu washiriki;***

Nimefurahishwa sana na kauli mbiu ya Kongamano hili isemayo *"**toa fursa ya kujieleza, badilisha mtazamo: Jenga mustakabali endelevu kwenye Sekta ya Habari katika zama za kidijiti**"*. Kauli mbiu hii pekee yake, imeshaelekeza mabadailiko ndani ya sekta ya habari. Kama kauli mbiu inasema hivi, ina maana wote tugeuke twende uelekeo huo. Kwa maoni yangu Kauli Mbiu hii imekuja wakati muafaka, hususan ikizingatiwa changamoto

nilizozieleza za mabadiliko makubwa ya kiteknolojia yanayoendelea kushamiri kote duniani, tunapaswa kuyakabili na sio kuyakimbia au kubaki tulivyo.

Katika zama hizi za "uandishi wa kijamii" *(social journalism),* ambao mara nyingi umegubikwa na habari zisizo za kweli *(fake news/misinformation),* Kauli Mbiu hii inakupeni fursa ya kutathmini na kutafakari namna ya kwedana na uhalisia huo wa Dunia ya sasa *(co-existence)*. Endapo wanahabari mkibebwa na upepo wa ***social journalism,*** mnaweza kujikuta mnaharibu heshma na murua wa uandishi wa habari na kuzua taharuki zisizo za lazima, na pengine kuleta maafa. Mnajua, jamii yetu inapenda sana mambo yenye ukakasi, akisoma jambo kama hilo kwenye mtandao au kwenye gazeti, analiamini hata akipewa ufafanuzi na taarifa sahihi, bado anang'ang'ania alichokisoma gazetini au mtandaoni. Ninyi mnafahamu zaidi kwamba***, kalamu ina makali kuliko panga***. Upanga utamkata mtu mara moja, lakini kalamu ukiandika inaweza kuathiri watu wengi zaidi. Kwa hiyo, jitahidini kutumia kalamu zenu vyema kwa manufaa ya umma lakini kwa manufaa ya Taifa letu.

Faraja yangu ni kwamba, miongoni mwa mada mtakazojadiliana zitahusu uendelevu na ustahimilivu wa vyombo vya habari; lakini pia zitahusu demokrasia na uhuru wa kujieleza katika zama za kidijiti; uandishi wa habari wenye uwajibikaji kama nilivyosema mwanzo; lakini pia wajibu wa vyombo vya habari katika kuripoti mchakato wa uchaguzi; usambazaji na matumizi ya matokeo ya sensa; na fursa ya changamoto za Akili Bandia ***(Artificial Intelligence).*** Siku hizi limezuka neno ***Akili Mnemba****,* nimewahi kumuuliza mtu,

‘mnemba maana yake nini, imeanzia wapi, na ni lugha gani?’ *nikaamibwa sijui ni neno lina asili ya kinyiramba, sijui wapi?*; nikamwambia kwetu, Mnemba ni majina ya watu, lakini pia ni jina la kisiwa huko kama unaelekea Pemba. Kwa hiyo ukiniambia Akili Mnemba kidogo inanichanganya, lakini ukisema Akili Bandia, naelewa ni ***Artificial Intelligence***.

Katika uendelevu na ustahimilivu wa vyombo vya habari, lazima tukubaliane kwamba zama zinabadilika, na hivyo lazima vyombo vyetu viendane na mabadiliko hayo. Utoaji wa habari umehamia kwenye mitandao sasa hivi, kwa wanangu kina Maxence Melo, kwenye *Jamii Forums*, *Tanzania Leaks* na kadhalika. Huko ndiko kunakovujishwa mambo yote. Sasa wale wanangu wa JUMIKITA, kwanza nakushukuruni kwa kazi nzuri mnayoifanya, lakini mnawajibu sasa wa kujichuja huko, kuhakikisha uhuru wa mawazo upo, mtu aandike anavyotaka. Sasa kuwaelewesha wale wengine wanaoandika wanavyotaka, tutumie uhuru wetu kuijenga nchi yetu, si kubomoa nchi yetu. Watu wakisoma nje tunajibomoa wenyewe na sifa yetu Tanzania wanayoijua, hawatuelewi.

Kwa hiyo JUMIKITA wanangu hebu mkafanye kazi nzuri. Makongamano haya yanakupeni fursa ya kujitathmini. Kwa hiyo na katika vyama vyenu, kaeni mjifanyie tathmini muone, kazi zenu zinaleta matokeo gani kwenye jamii. Matokeo hasi hayakosekani, lakini yanaathiri kiasi gani nchi yetu?

Nitilie mkazo uchambuzi wa habari. Mimi huwa namfuatilia sana mdogo wangu, Mkurugenzi Mkuu wa TBC ambaye huwaalika wataalam mbalimbali

kuchambua masuala mbalimbali yanayotokea nchini. Lakini nikisoma habari magazetini, habari za uchambuzi ni kidogo sana. Habari zilizopo ni za kutaarifu tu, hazifuatiwi na uchambuzi wa kina. Tunahabarisha zaidi kuliko kufanya uchambuzi (*reporting rather than analysing)*, nadhani tuna uhaba wa wachambuzi wa habari. Mtu anachukua taarifa kama alivyoipokea na kuichapisha bila uchambuzi wowote. Ukisoma unajiuliza kama kweli aliyeandika ni mwandishi wa habari na kama alipata muda wa kujiuliza baadhi ya maswali.

Niseme kwamba, jielekezeni kwenye habari zinazokubalika, pamoja na kwamba, pengine zinaweza zisiwape umaarufu mkubwa. Ukiangalia wenzetu, waandishi wanaandika habari zinazokubalika, kwa uwazi na zenye kuaminika, (Clean, transparent and reliable news). Ukifanya uchambuzi, habari yeyote unaweza kuiandika unavyotaka wewe, na anayeisoma akaiamini taarifa yako. Kwa hiyo. Mhe. Waziri na Bwana Tido na wabobezi wenzako, wasimamieni wenzenu. Ni matarajio yangu kwamba, mwisho wa Kongamano hili mtakuwa mmeongeza maarifa na ujuzi kuhusu sekta yenu katika zama hizi zenye wingi wa utata wa habari.

Lakini kwa upande mwingine, kuna wingi wa utata wa habari unaokabili nchi yetu. Kuna shutuma zinaibuliwa dhidi ya nchi yetu, ambazo sio za kweli. Sasa Waandishi wa Habari badala ya kuchukua zile tuhuma, kuzifanyia uchambuzi na kupata ukweli halisi, ninyi mnaandika kama mlivyosikia. Unapoandika kwa fahari kuhusu yanayoibuliwa na vyombo vya nje, wala haumchafui Samia, unaichafua nchi, ambayo na wewe ni sehemu yake.

Kwa hiyo, sisi wenyewe tuwe wafafanuzi wa hoja tunazopigwa nazo badala ya kuzishajihisha tena bila ya utafiti au uchambuzi wowote. Nadhani tuwe walinzi sisi wenyewe kwanza. Wakiona wanayoandika yanapata ufafanuzi kutoka kwa waandishi wenyewe hapa nchini, watakuwa makini katika namna wanavyoiaindika nchi yetu.

***Ndugu zangu wanahabari;***

Nizungumzie kidogo kuhusu Kamati ya Kufanya Tathmini Utendaji na Uchumi wa Vyombo vya Habari Tanzania Bara, iliyoongozwa na Bwana Tido Mhando. Nataka niwapongeze kwa kazi kubwa na nzuri mliyofanya. Nimpongeze Waziri kwa kuunda Kamati hii, na inanipa moyo, kwa sababu ametumia staili yangu ya utendaji kazi kwa masuala magumu na mtambuka. Lakini pia inaonesha ujasiri wa kujitathmini wenyewe, tumekuwa wakweli, tumehojiana, tumekusanya masuala yanayowasibu na kuainisha yale ya kutekelezwa na Serikali na yaliyo ndani ya uwezo wenu wenyewe. Kwa hiyo, mimi niwapongeze sana kwa hatua hii ya kujitathmini. Bwana Tido na Kamati yako hongereni sana.

Nilikuwa nasikiliza kwa makini sana wakati hoja zinawasilishwa. Niseme kwamba taarifa hii imeweka msingi mzuri wa majadiliano ambayo mtakuwa nayo kipindi hiki cha leo na kesho ambacho mpo kwenye mijadala yenu. Kuna mambo kule mkiyachukua, mtaweza kuyajadili wenyewe na mtakuja na suluhisho wenyewe, sisi mtatuletea taarifa kwamba, kwenye hili tunadhani suluhisho ni hili, kwa hiyo na sisi tutaangalia uwezo wetu na kuamua namna ya kutekeleza. Pamoja na yaliyoandikwa na mtakayoyajadili, mimi niache maagizo kwa Mheshimiwa

Waziri na Timu yako hii iliyoandika Taarifa, muendelee kufanya uchambuzi wa Taarifa yenyewe na muiwasilishe Serikalini ili tuweze kuchukua hatua.

Nigusie machache ambayo yamesemwa hapa, la kwanza ni madeni. Hili ni suala la muda mrefu, lipo, nimeshakutana nalo mara nyingi. Tulianza kufanya uhakiki wa madeni ya vyombo vya habari, kuna madeni yanayolipika na yana ushahidi, lakini kuna yasiyo na ushahidi. Nilipozungumza na Wahariri, kina Machumu na wenzake, waliniambia, moja ya changamoto zilizokuwa zinawakabili ilikuwa ni madeni yao ambayo yalikuwa hayalipwi kutokana na kukosa ushahidi. Nikawauliza 'kwa nini hayana ushahidi?' wakanifahamisha kwamba walikuwa wanapigiwa simu za maombi kuwataka watoe tangazo bila maandishi. Hakuna nyaraka yoyote, na unataka Serikali ilipe. Inalipa kuanzia wapi? Bahati mbaya ni mengi sio kidogo, lakini hayalipiki kwa msingi huo. Kwa hiyo tukatafuta njia mbadala, ambayo ilikuwa kuyasogeza mashirika yetu karibu na vyombo vya habari ili basi yavishike mkono na kupunguza machungu kidogo.

**Kwa madeni yaliyokwishafanyiwa uhakiki na yanalipika, niwaahidi kwamba tunakwenda kuyalipa.** Lakini tukijiuliza msingi wa madeni haya, mimi nadhani ni kutokana na vyombo vyetu kutoendeshwa kibiashara. Sidhani kama makampuni makubwa kama IPP Media yana madeni makubwa Serikalini, kwa sababu wao wanajiendesha kibiashara. Lakini katika vyombo ambavyo, Mkuu wa Chombo ni Mwanahabari mwenyewe huyo huyo, ni nadra kuwa na mtazamo wa kibiashara, mtazamo wake ni habari zaidi. Ndio maana akipigiwa simu nitolee habari hiyo, anaharakisha anatoa; hadai barua, hadai risiti, hadai *invoice*, hadai

chochote anakwenda tu anatoa. Sasa nadhani tubadilike, vyombo vyetu viendeshwe kibiashara.Vikiendeshwa kibiashara haya madeni hayatakuwepo. Kwa sababu kama TRA anakudai na wewe utamdai kwa uhakika uliyemtolea matangazo yake.

Kuhusu lile ombi kwamba TRA wasiwadai mpaka mlipwe kwanza, TRA hiyo ndiyo kazi yake, mkitaka afanye kama mnavyofanya nyie mpaka ulipwe miezi sita ijayo na yeye ndiyo akudai VAT hapana, watakuwa hawajafanya kazi yao, atakudai palepele kwa sababu ndiyo kazi yake. Akiona muamala, naye atadai kodi yake. Sasa nadhani tubadilike na sisi tufanye kazi kibiashara kuliko kwa kujuana. Mkiwagomea mara mbili, mara tatu hawataleta matangazo bila kulipa; watalipa kwanza ndio walete.

Suala jingine, hili la uwekezaji kutoka nje ni takwa la sheria, na kwa vile mmelileta tunakwenda kuliangalia, kwamba tuongeze kile kiwango cha hisa za wawekezaji kutoka nje. Ni kweli kwa sababu vyombo vingi ambavyo vilikuwa na watu wa nje wamerudi nyuma, na kwa hiyo vile vyombo vimepunguza kufanya kazi. Kwa hiyo tutaliangalia. Kuhusu suala la Mfuko wa Mafunzo ya Habari (*Media Training Fund),* tusubiri ianze kwanza na tuone inavyofanya kazi, halafu ndio tuibebeshe mizigo mingine. Kama sheria inaruhusu (kuongezea) mfuko huu (majukumu mengine), mfuko utakuwepo; (kwa sasa) ngoja tuanze, tuutilie fedha, tuanze kuuendesha halafu tuendelee na mambo mengine.

Kuhusu maudhui salama na athari zake, tumezungumza, kwamba, tujiangalieni tunachokifanya. Maudhui salama yataiweka nchi yetu vizuri, maudhui mabaya ya ovyo, ya shari, yatakuwa ndio huo upanga unaosemwa, tunajiwekea wenyewe.

***Ndugu zangu***;

Kama mnavyofahamu, Sekta ya habari ni muhimu katika kukuza demokrasia, uwazi na uwajibikaji katika jamii yetu. Kadri nchi yetu inavyokua kiuchumi, ni lazima na mifumo ya kuendesha mambo yetu ibadilike; tunavyokuwa na kila kitu kinatakiwa kubadilika. Namna ya kuishi kistaarabu ni pamoja na kuwa tayari kusikia mawazo kinzani. Hapa simaanishi kashfa, kebehi na matusi, hapana. Mawazo kinzani tu. Serikali inakuja na hili na kuna mwingine anawaza jingine tuko huru kusema 'hapana, sisi tunadhani kuliko hili lililoletwa na Serikali lingekuwa hili', ambapo tunafanya vizuri sana tunasema. Lakini simaanishi kwamba, tunaposema uhuru wa kujieleza, uhuru wa vyombo vya habari, basi mtu mmoja asiye na malezi kwao huko asimame tu aanze kukashifu, aanze kutukana, kuporomosha matusi, aanze kukebehi; hatumaanishi hivyo. Watanzania hatuko hivyo.

Mimi ninaamini Mtanzania ambaye amekuwa kwenye maadili ya kitanzania kusimama na kutoa matusi, tunamshangaa na kujiuliza sana. Sasa, tunaposema uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza, kuna mipaka yake. Kuna wengine hawana moyo wa kubeba wanapokashifiwa na kurushiwa matusi, ndiyo pale tunaposema kalamu yako ulichokiandika kinakuwa upanga

sasa, kinaleta shida, kinaleta mizozano. Kwa hiyo tunaposema uhuru wa kujieleza simaanishi hayo mengine yanayojitokeza kwenye jamii yetu, namaanisha majibizano ya hoja kama nilivyosema, mmoja anakuja na hoja hii mwingine anakuja na hoja mbadala, tunaboresha na kusonga mbele. Wote kwa pamoja tukienda hivi tutafika mbali. Kwa sababu nikikusikia napata kurekebisha kwangu, na nikirekebisha nakaa vizuri keshokutwa nikisimama jukwaani kuomba ridhaa, huwezi kuja kunisuta.

Sasa, wakati tunasubiri kama nilivyosema, ripoti ile Wizara waichakate na watuletee niache maagizo yafutayo:-

a) Wizara na Taasisi za Umma zote zinazodaiwa na vyombo vya habari ndani ya Serikali yangu, zihakiki madeni ya vyombo hivyo, na kuhakikisha zinakubaliana utaratibu wa malipo. Jambo hili lifanyike si zaidi ya Disemba, 2024. Tukivuka 2025 madeni mengi ya vyombo vya habari yanayolipika yawe yamelipwa.

b) Vyombo vyote vya Habari vitoe kipaumbele, mtakapokuwa mnalipwa, na nyinyi lipeni wafanyakazi.

c) Kuhusu mikataba ya ajira, wanasema mfinyanzi hulia magaeni. Waandishi nyinyi ndio mahodari wa kuandika mashirika yasiyokuwa na mikataba, mashirika yanayochelewa kulipa mishahara, sijui taasisi zinazochelewa kufanyaje. Sasa ninavyosikia leo hii hapa kwamba hamlipwi na hamna mikataba na mmenyamaza kimyaa, hamsemi. Nikasema kweli mfinyanzi hula kwenye magae; yeye ni mfinyanzi anafinyanga vyungu, anauza, mwenyewe anakula kwenye magae. Poleni ndugu zangu. Nadhani mngeamua kusema mabosi

wangeshtuka wangekulipeni lakini mmebana kimyaa, ndiyo ile wanasema 'ya kwao duu ya wenzenu midomo juu'. Haya sisi tutawasaidia.

Jingine Mheshimiwa Waziri, Wizara iendelee kuhamasisha ubunifu na teknolojia katika sekta ya habari. Kwa sababu enzi tulizo nazo hizi hatuwezi kurudi nyuma, lazima tuendelee na ubunifu na matumizi ya teknolojia. Nilikuwa nasikiliza hapa malalamiko ya VAT kwamba, mbali ya yale yaliyosemwa kwamba tusidaiwe lakini nakumbuka nilishapata malalamiko ya VAT kuhusu karatasi za magazeti, zipunguzwa au zifutwe kwa sababu magazeti hayauziki. Ni kweli, magazeti hayauziki, kwa sababu wasomaji wamepungua; sasa hivi tunasoma kwenye mtandao. Wasomaji wa magazeti ya makaratasi wamepungua mno. Kwa hiyo wenye biashara ya magazeti lazima kubadili mbinu za kibiashara, fanyeni tathmini 'je muendelee na biashara ya magazeti, au mfanyeje?. Jingine ni kwamba hata malighafi ya karatasi za magazeti inatoka kule kwenye vita ambapo sasa hivi hawashughuliki kupeleka karatasi za magazeti wanashughulikia na mambo yao. Hebu jiangalieni tena wale wa biashara ya magazeti turekebishe kitu gani au tuende vipi ili biashara iendelee kusimama.

***Ndugu washiriki;***

Mtambue kwamba, taarifa sahihi za nchi yetu ni muhimu zikawafikia wananchi. Leo nimefurahi kwamba zimetolewa tuzo na kuna Halmashauri zimeshinda kwenye hizo tuzo. Hizi ni Halmashauri ambazo zina redio zao za

jamii kule na pengine wanapeleka taarifa kule, taarifa ile ya redio za jamii ikijirudia wananchi wanapata kujua.

Lakini, nimesikia hapa waandishi wa habari za vijijini. Kuweni kweli waandishi wa habari za vijijini. Unakuta taarifa za vijijini zinarushwa zaidi kwenye vyombo vya kitaifa lakini kule kwenye redio za jamii hazipo na wananchi hawazisikii. Kama (wananchi) wakisikia leo kamati ya siasa ya Wilaya yao wametembelea miradi ulioko kwenye Wilaya yao, wamekuta kasoro au wakaisifia Serikali kwa kufanya kazi nzuri ya kujenga shule, wananchi wangekuwa wanasikia kule lakini, ikishapelekwa TBC, ITV, UTV inaonekana inatosha. Kwa hiyo kwa zile Halmashauri zinazofanya hivyo na zikatuzwa leo, endeleeni kufanya hivyo na zile ambazo hazifanyi, huu ndio unatakiwa kuwa mwelekeo. Kwa hiyo sambazeni hizi taarifa muwatendee haki wananchi. Lakini pia mtendee haki dhamana zenu mlizopewa hii ndiyo kazi yenu, ndiyo kazi yenyewe. Kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu tendeni haki nendeni kafanyeni hayo.

Nimeona, Halmashauri ya Temeke ya Dar es Salaam imekuwa mshindi wa kwanza, wanayo kila sababu ya kuwa washindi wa kwanza. Vyombo vyote vya habari vipo Dar es Salaam; TV, Magazeti, Redio vyote vipo Dar es Salaam. Sasa nadhani ipo haja ya kuboresha zaidi vigezo vya upimaji (assesment criteria) ili majiji yapimwe peke yake, miji na mikoa ya pembezoni nayo ipimwe peke yake. Pili nipendekeze pia sekta nazo zishiriki. Leo nimesikia Idara za Maji zimeshiriki kwenye Tuzo kwamba Maafisa Habari wao wanaotoa habari kuhusu sekta yao.

Sasa tanueni wigo, ili sekta nyingine kama kilimo, viwanda na biashara nazo ziseme nani anatoa taarifa zao vizuri. Zieni nafasi sekta nazo zijisemee, kwa sababu kuna sekta hapa leo hazikutajwa kabisa. Kwa hiyo nadhani na sekta nao wapeni fursa wachague mtu gani anatoa taarifa zao vizuri.

Jingine ninalotaka kuwaachia kama nilivyosema redio jamii na zenyewe zishughulikieni ili taarifa ziende huko. Lakini pia toeni ushauri kwa Viongozi, na hii ni kwa Maafisa Habari hasa wale wa Wizara na Mashirika. Toeni ushauri kwa viongozi na maafisa wengine Serikalini kuhusu mbinu bora za mawasiliano na njia za kuboresha ufanisi wa utoaji taarifa kwa umma.

Kwa wale waandishi wa Mashirika na Wizara, la muhimu zaidi kwenu, ni kuzielewa vizuri sera na vipaumbele vya Serikali halafu mkaoanishe ndani ya kazi yenu. Kuna baadhi yenu hata kwenye sekta zenu wenyewe hamjui vipaumbele vya kisekta. Sasa kama hujui vipaumbele vya sekta yako utafanya kazi vipi? Ijue sekta yako kisera, vipaumbele vyake halafu andika. Fanya uchambuzi wa utekelezaji, umekwama wapi, changamoto ni zipi, siyo vibaya kuweka changamoto kama Wizara yako imeshindwa kutekeleza sema changamoto ni hizi.

Kuna changamoto ninaiacha kwenu, nawaachia kazi ya kufanya, mtuletee mapendekezo ya kuundwa kwa Mkakati wa Mawasiliano Nchini (National Communication Strategy). Mhe. Waziri kama utaunda Timu nyingine ya hii, tukaiangalie

*Ndugu zangu;*

Nikihitimisha nirejee wito wangu kuhusu umuhimu wa uwajibikaji katika uandishi wa habari. Kama tunavyofahamu, mwaka huu tunaanza na hagUchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kalamu zenu zitakwenda kufanya kazi kubwa humo; sasa kafanyeni kazi itakayojenga na sio kazi ya kubomoa.

Unajua katika nchi zetu zinazoendelea kipindi cha uchaguzi ndiyo kipindi cha kujenga hofu za watu, lakini kumbe tukifanya kazi yetu vizuri tukiandika vizuri, ni kipindi cha kuwaelekeza watu na kuwapa taarifa za vyama vyao. Chama gani kinafanya vizuri wapi, chama gani hakifanyi vizuri wapi, ili wajitutumue na wenyewe wakafanye vizuri. Mnaruhusiwa kuvichambua vyama vya siasa, kutuandika na wenzenu ndiyo wanavyofanya. Lakini hatuendi hadi kuvigonganisha vyama na kuleta vurugu ndani ya nchi. Wenzenu hawafanyi hivyo. Nyinyi msitumike kufanya hivyo. Kwa maneno mengine **Msitoboe dau tunalosafiria ndani ya hilo dau tuko wote, ukitoboa yakiingia maji tukizama tunazama wote.** Lakini pia labda niseme **msiingie kwenye mtego wa kurarua nyuzi zilizounganisha kitambaa cha Taifa letu. Kwa hiyo mimi niwaombe sana ndugu zangu nyinyi ni watu muhimu sana kwa usalama na utulivu wa Taifa letu.**

Jingine ni la stara tu. Unajua mara nyingi tukimuomba Mungu, tunamuomba atujaalie afya, uzima, nguvu na stara. Sasa wewe kama binadamu mmoja unataka stara lakini nchi yetu hatuistiri. Aibu ya nchi yetu ndugu zangu nyie ndiyo mtakapokaa kuzichonga na mkazipangilia vizuri kisha mkarusha nje

huko. Mnaifungua, mnaifunua, sasa wewe chukulia lile jambo kama ni la kwako. Sasa msiingie kwenye mtego huo wa kugharimu nchi yenu ndugu zangu. Tumieni kalamu zenu kwa weledi, na kuuelimisha umma kuhusu haki na wajibu wao kwa nchi yao. Katika kipindi hiki cha uchaguzi, waelimisheni wapiga kura haki na wajibu wao, umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi, kuripoti vitendo vya rushwa vinavyotokea. Kwenye chaguzi huko kuna mambo mengi, mkiyaona semeni, kwenye uchaguzi huku kuna hili na mmefanya hivyo miaka ya nyuma.

**Baada ya kusema hayo ambayo nimesema niwaombe sana twendeni tukadumishe utulivu na amani ndani ya nchi yetu na pia niendelee kuwahikishia kuwa, vyombo vya habari sio mshindani wa Serikali, bali ni mshirika (*partner*) wa Serikali. Tunafanya kazi pamoja ili kujenga Taifa imara la Tanzania lenye uwajibikaji, kuzingatia haki na Taifa la wachapa kazi. Kama tutawapa taarifa vizuri watanzania watachapa kazi.**

Baada ya kusema hayo, nitamke kwamba Kongamano la Pili la Maendeleo ya Sekta ya Habari, sasa limefunguliwa rasmi. Niwatakieni majadiliano mema.

**Niwashukuru sana kwa kunisikiliza.**